RULENGE - NGARA CATHOLIC DIOCESE

Biharamulo Health Sciences Training College
BHSTC (School of Medical Lab Sciences)

Box 43, Biharamulo, Kagera. Tel: 0765-158479, 0752835813, 0784638491,
Email: bhstcollege@gmail.com Website: www.biharamulohstc.ac.tz

MZAZI/MLEZI/MFADHILI WA

……..

……..

……..

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MAABARA
KOZI YA MIAKA MIWILI KUANZIA TAREHE 01/10/2022.

Napenda kukupongeza, kwa kuchaguliwa kujiunga na kozi ya Uteknolojia maabara kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

1. a) Chuo hiki ni mali ya Jimbo katoliki la Rulenge Ngara, ambacho kimesajiliwa na NACTE kwa namba **REG/HAS/121. Usajiri Kamili. (Full Registration)**
   b) Masomo yanachukua miaka miwili (2) ngazi ya Cheti
   c) Mwanachuo baada ya kufuzu masomo yake anasajiliwa kama Mteknologia msaidizi na kutunukiwa Cheti cha Mteknolojia msaidizi maabara.
   d) Ushirikiano ni muhimu sana ili mwanachuo aweze kufuzu masomo yake kwa muda uliopangwa ambao ni miaka miwili (2)

2. **LENGO:**
   Kumwandaa mwanachuo katika elimu bora,kumlea katika maadili mema na kumuelekeza katika utendaji kazi bora ili aweze kuwa wa manufaa kwa jumuiya nzima na taifa la Tanzania.

3. **MAHITAJI MUHIMU YA MWANACHUO**
   Mwanachuo kabla ya kuanza lazima awe na vifaa hivi vifuatavyo: -
   A. Afike na “Pay in slip” ya Malipo na yafanyike bank.
      1. Sare ya Chuo

WAVULANA

- SULUARI KHAKI 2
- SHATI NYEUPE 2
- SWETA KIJIVU 1
- MEDICAL COAT NYEUPE 1

WASICHANA

GAUNI NYEUPE 2
SWETA KIJIVU 1
MEDICAL COAT NYEUPE 1

B. VIFAA VYA MASOMO

- Daftari za kutosha
- Karatasi (Ream) 1 kila muhura (Double A).
- Kalamu za wino, risasi, rula na kifutio
- Kalamu za rangi mbalimbali za kuchorea
- Kamusi ya Kitabibu (medical dictionary)

C. VIFAA VINGINE: -

- Chandarua 4x6x7 ft 1
- Blanketi 1
- Mashuka urefu mita 2.5 upana 1.5 4
- Viatu vyeusi/ kahawia vilivyofunika, viwe vya Ngozi jozi 2 vya kufunga kamba au visivyofungwa kamba viwe vinafunika miguu sio vidole tu, visiwe na visigino virefu wala vifupi sana, wala kuchomoza/ kuchongoka mbele.
- Ndoo ya plastic yenye mfuniko, ujazo wa lita 20 moja. (1)
- Beseni 1
- Nguo za michezo jozi moja (1) rangi ya Bluu wasichana na Rangi Nyekundu kwa wavulana
- Viatu vya michezo raba au njumu
- Tochi yenye betri (wakati wa dharura)
- Mwavuli au koti la mvua
- Matumizi ya lazima ikiwa ni pamoja na Pesa za kujikimu (pocket money).

4. Mwanafunzi afike ofisi ya Utawala Chuoni akiwa ametia sahihi katika sehemu ya Sheria na Kanuni za Chuo.
5. Tarehe ya kufungua chuo ni 01/10/2022 kati ya saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.

MALIPO YA MWAKA WA KWANZA

****KARO INARUHUSIWA KULIPWA KWA AWAMU 4**

1	TUITION FEE	1,500,000
2	ACCOMODATION / HOSTEL	200,000
3	FIELD WORK	250,000
4	INTERNAL EXAMINATION	200,000
5	TREATMENTS	100,000
6	CAUTION MONEY	20,000
7	IDENTITY CARD	10,000
8	STUDENT ORGANIZATION	10,000
9	REAGENTS	100,000
10	INTERNET	50,000
11	GRADUATION	25,000
12	QUALITY ASSURANCE	15,000
13	PROCEDURE BOOKS	20,000
JUMLA		**2,500,000**

***Mwanafunzi atajigharamia Chakula muda wote awapo chuoni. Chakula kinapatikana maeneo ya chuo kwa gharama nafuu na elekezi. ***

**GHARAMA ZA MITIHANI YA WIZARA (Hulipwa kila mwaka moja kwa moja wizarani)	
Mwaka wa kwanza = 150,000/=	Mwaka wa Pili = 150,000/=

Utaratibu wa malipo utakuwa kama Vifuatavyo kwa mwaka wa kwanza

AWAMU YA KWANZA	AWAMU YA PILI	AWAMU YA TATU	AWAMU YA NNE	JUMLA
700,000/=	***650,000/=***	***600,000/=***	***550,000***	***2,500,00/=***

Fedha yote ipitie Benki, Jina la mwanachuo ndilo litakaloandikwa kwenye HATI YA MALIPO.

Jina la Akaunti**: -** **BIHARAMULO D.D.H**

Akaunti No. **NMB 31706600267**

Hatupokei pesa tasilimu wala hundi, tunachopokea ni **HATI YA MALIPO** ya Benki.

****NAKUTAKIA MANDALIZI MEMA****

PRINCIPAL
SCHOOL OF MEDICAL
LABORATORY SCIENCES
P.O.Box 43 - BIHARAMULO

BENJAMIN. R. KIMWAGA

MKUU WA CHUO.

SHERIA NA KANUNI ZA CHUO

1. Kuamka mapema na kutandika kitanda ,kuoga na kufanya usafi wa chumba cha kulala
2. Kila Mwanachuo ahakikishe anatunza usafi wa mavazi yake, mwili wake pamoja na chumba cha kulala, choo,bafu na mazingira kwa ujumla ikihusisha mabweni na shuleni.
3. Kuwa darasani wakati wote na saa za mafunzo na kufuata Ratiba
4. Kuvaa nguo nzuri na za heshima owapo darasani,chuoni na hata nje ya chuo
5. Kwa kuwa hiki ni chuo cha kanisa Katoriki, Kila Mwanachuo atatakiwa kuhudhuria sala kila asubuhi ,na siku za vipindi vya dini kwa dhehebu lake.
6. Kila Mwanachuo atatakiwa kuwa na nidhamu na sifa nzuri awapo chuoni na nje ya chuo.
7. Ugomvi , matusi na lugha chafu havitakiwi chuoni, Mwanachuo ajenge uhusiano mwema na Wanachuo wenzake, Walimu na wafanyakazi wote.
8. Ni marufuku kwa Mwanachuo kushiriki jambo lolote linalovunja amani chuoni ikiwa ni migomo pamoja na mikutano isiyo rasmi. Atakaye fanya hivyo ataondolewa chuoni mara moja.
9. Ni marufuku kwa Mwanachuo kula chakula nje ya eneo / kantini iliyotengwa maalumu kwa chakula bora cha wanachuo wote.
10. Mwanachuo haruhusiwi kutoka nje ya eneo la chuo bila ruhusa.
11. Kuwa mwangalifu na kutunza mali na vifaa ulivyokabidhiwa na chuo kwa matumizi yake
12. Wizi ni marufuku, Mwanachuo atakayebainika kuwa na tabia hizo atafukuzwa kozi mara moja.
13. Ni marufuku kwa mwanachuo kujihusisha na mapenzi awapo chuoni
14. Mwanachuo atakayepata mimba akiwa chuoni haruhusiwi kuendelea na masomo
15. Ni marufuku kuvuta sigara au kutumia pombe na madawa ya kulevya uwapo chuoni na nje ya chuo.
16. Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote chuoni bila ruhusa maalumu.

Mimi, ……. Nimesoma na kuelewa kanuni na sheria za chuo. Naahidi kuzitekeleza kwa kipindi chote cha kozi yangu ya mafunzo ya Maabara niwapo Chuoni. Nikikiuka kanuni na sheria hizo, hatua za kinidhamu zichukuliwa dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

Jina la Mwanachuo: …… Saini ya Mwanachuo …….

Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanachuo……

Saini ya Mzazi/Mlezi wa Mwanachuo: …….

Utaratibu wa Fomu ya Uchunguzi **(**Medical Exiamination form) utafanyika mara tu mwanafunzi anaporipoti Chuoni ktk hospitali ya Biharamulo DDH.